TANGAZO LA SERIKALI Na. 223 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA BUZIKU YA MWAKA 2023

Jina

**1**. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Buziku ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa
eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

**3**. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 327855.3206MS, 9692174.4872KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $105^0$ kwa umbali wa kilomita 17.37 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 328955.9895MS, 9693518.5733KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $118^0$ kwa umbali wa kilomita 2.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 331612.4115MS, 9692999.9889KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $133^0$ kwa umbali wa kilomita 3.26 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 333326.9149MS, 9690227.1500KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $121^0$ kwa umbali wa kilomita 1.94 hadi

kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 332427.3298MS, 9688502.0632KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $87^0$ kwa umbali wa kilomita 3.94 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 329025.2223MS, 9690492.6158KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $155^0$ kwa umbali wa kilomita 2.04 hadi ulipoanzia.''

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*